# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 029 ISSN 1821 - 8253 NOVEMBA 2016



## ZANZIBAR INAVYOSHUHUDIA MABADILIKO MAKUBWA KATIKA SEKTA YA AFYA

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Said J.Ameir

**Waandishi**
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed


## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.


Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.



P.O.BOX: 2422
Zanzibar - Tanzania
Phone: +255 223 0814/5
Fax: 024 223 3722
Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz


# Maoni ya Mhariri

## Hatimaye tumepata tulichokitaka

Tarehe 15 Novemba, 2016 Zanzibar iliandika tena katika vitabu vya historia yake tukio kubwa ambalo bila ya shaka yoyote limeleta matumaini mapya na makubwa ya kujenga mustakbala mwema na imara wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Zanzibar kwa miaka mingi ijayo.

Ni tukio la kuhitimisha mchakato wa muda mrefu wa kutunga Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar ambao umekamilishwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa kutia saini Sheria hiyo Namb. 6 ya mwaka 2016 mbele ya viongozi mbali mbali wa Serikali na waandishi wa habari.

Sheria hii inaipa Zanzibar mamlaka ya kutafuta na kuchimba mafuta na gesi asilia ambayo hapo awali haikuwanayo kutokana na sheria zilizokuwepo kuipa mamlaka hayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika lake la uchimbaji mafuta TPDC pekee.

Ni ukweli kuwa hadi kufikia hatua ya kutiwa saini sheria hiyo kulikuwepo na mazungumzo ya muda mrefu kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu suala la mafuta na gesi kuondolewa katika orodha ya mambo ya Muungano.

Ni kitu cha kujivunia na kumshukuru Mwenyezi Mungu kuwa mashauriano hayo yalifanyika katika mazingira ya udugu, urafiki na mshikamano ambao lengo lake lilibaki katika kutafuta mustkabala mwema wa watu wa pande mbili hizi za muungano.

Kwa hivyo ni wajibu wetu kuwashukuru viongozi wetu waliosimamamia suala hili hadi kufikia hatua ambayo wananchi wa Zanzibar wamepata na kuridhika na kile ambacho walikuwa wakikililia kwa miaka mingi.

Hatuna budi kuwashukuru viongozi wetu wa kitaifa kwa busara zao hadi kufikia hatua hii. Tunampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake imara uliojaa busara, hekima na uvumilivu na zaidi imani yake katika uongozi wa pamoja ambapo hata wakati mmoja katika masuala makubwa ya nchi hakuacha kuwashirikisha viongozi kupitia kwenye vikao rasmi vya maamuzi.

Safu hii ya Mhariri inaamini kwa dhati kabisa kwa kuwa changamoto ni suala la lazima katika mchakato wa maendeleo, zilikuwepo changamoto kadhaa katika hatua za mashauriano, lakini busara umahiri na umakini mkubwa wa Dk. Shein katika uongozi hatimae imefikiwa hatua ya kutiwa saini sheria hiyo tukio ambalo limepokelewa kwa shangwe na vigelegele na wananchi wa Zanzibar hasa wapenda maendeleo.

Aidha, ni wajibu wetu pia kumshukuru kwa namna ya pekee Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Jakaya Mrisho Kikwete kwa busara zake na uongozi wake thabiti katika kulishughulikia jambo hili.

Utayari wake tu ndio uliowezesha jambo hili kufanyika kwa namna lilivyofanyika. Angeweza, kwa wakati aliokuwepo, kusema suala hili aliahirishe limsubiri Rais ajaye kwa vile liliendelea hadi karibu na kufikia ukingoni mwa uongozi wake. Alitumia busara ya kiuongozi pamoja na uungwana kwa kuangalia haja na mahitaji ya ndugu zake wa Zanzibar katika kujenga na kuimarisha uchumi wao.

Dk. Kikwete alielewa fika kuwa 'fursa haiji mara mbili' hivyo ilikuwa ni wakati muafaka kwake kuuharakisha mchakato ule hadi Bunge likapitisha Sheria Mpya ya Mafuta Namb. 21 ya mwaka 2015 ambayo inaipa uwezo Zanzibar kushughulikia masuala ya mafuta na gesi asilia kwa kutumia sheria itakazozitunga yenyewe. Katika mtazamo huo huo, Dk. Kikwete hakufanya ajizi akatia saini Sheria hiyo tarehe 5 Agosti, 2015.

Zanzibar sasa ina sheria yake ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa lugha za wenzetu wanasema sasa "mpira uko upande wetu". Tunatakiwa kuucheza! Kwa bahati nzuri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianza matarayarisho ya kuendeleza sekta hii muda mrefu baada ya kupata matumaini ya kuwepo mazingira ya sasa ya kuwa na sheria yake. Sera ilikwishaundwa na kupitishwa.

Ni kweli kuwa Sheria hii imeleta matumani kwa kila mwananchi wa Zanzibar lakini kama alivyotahadharisha Mheshimiwa Rais baada ya kusaini sheria hii kuwa isitegemewe kuwa manufaa ya sekta ya mafuta na gesi yatapatikana kufumba na kufumbua. La hasha, inaweza kuchukua miaka isiyopungua kumi lakini kubwa alilosisitiza ni ustahamilivu tena si kwa wananchi tu lakini hata kwa serikali yenyewe!

Alichomaanisha Mheshimiwa Rais ni kuwa bado kuna safari ndefu hadi kufikia hatua ya kufaidika na sekta hii na hata Sheria yenyewe inathibitisha hilo kwani inaanza na neno "kutafuta", ikimaanishwa kutaka kitu au jambo ambalo hulijui lilipo. Hivyo sijambo lililo tayari!

# Zanzibar inavyoshuhudia mabadiliko makubwa sekta ya afya

1



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Balozi wa China Nchini Tanzania Mhe. Lu Youqing wakikata utepe kuizindua Hospitali mpya ya Abdalla Mzee Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba. iliyojengwa kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, tarehe 26 Novemba. 2016

Kuishi kwingi kuona mengi, ni miongoni mwa semi za Kiswahili zilizozoeleka miongoni mwa waswahili hasa wazee waishio mwambao wa bahari ya hindi, ambao mazungumzo yao hujikita zaidi kwenye simulizi za matukio mbali mbali wakati wa enzi zao za utotoni hadi ujanani kwao.

Lakini simulizi za wazee wa miaka ya hivi karibuni hapa Zanzibar, zinahusishwa na mabadiliko makubwa ya kimaendeleo katika sekta tofauti ikiwemo sekta ya afya Unguja na Pemba, ambayo kama zilivyo sekta nyengine nayo imepata mafanikio ya kupigiwa mfano.

Vifaa vya kisasa vinavyotumika kutambua na kutibu maradhi mbali mbali ya mwanadamu katika hospitali za Unguja na Pemba, vinaonekana na baadhi ya wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea kuwa kama miujiza kutoka kwa Muumba.

Mara nyingi wanashindwa kumithilisha kwa mfano maumivu makubwa na ya muda mrefu waliokuwa wakiyapata wakati kwa bahati mbaya inapotokezea kufanyiwa upasuaji mambo ambayo kwa sasa yamebaki kuwa historia.

Wanakumbuka wanapojiona wakiwa na makovu makubwa yaliyoachwa na majaraha ya upasuaji mambo ambayo kwa mujibu wa teknolojia ya sasa yanaonekana kuwa ni mateso makubwa kwa binadamu.

Hatua ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wake bila ya ubaguzi, ni utekelezaji wa malengo makuu ya Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari 1964 ulioanza kuonekana tokea mara tu baada ya Mapinduzi hayo kufuatia kutangazwa matibabu kuwa bure kwa kila mtu.

Ni dhahiri hatua hiyo iliondosha unyonge kwa wananchi wa Zanzibar ambao wengi wao ni masikini na hawakuwahi kufaidika na huduma hizo zilizokuwa zikitolewa kwa ubaguzi kabla ya Mapinduzi.

Utekelezaji wa uimarishaji wa sekta ya afya umekuwa ukiendelea hatua kwa hatua ingawa mtikisiko wa uchumi duniani katika miaka ya 80, ulioyumbisha harakati za maendeleo katika bara la Afrika ikiwemo Zanzibar, ulidhoofisha pia huduma za afya Zanzibar pamoja na huduma nyengine za jamii. Kutokana na mtikisiko huo, Serikali ililazimika kubadili sera zake ili kuhakikisha kuwa huduma zote muhimu zinaendelea kupatikana vizuri kwa wananchi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Hauklend Bw. Eivend Hansen wakikata utepe kuzindua jengo la Wodi ya Watoto wakati wa uzinduzi wa majengo mapya ya Wodi ya Kinamama na Watoto uliofanyika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, tarehe 11 Novemba 2016

Katika jithada za kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilianzisha mpango wa ushirikishwaji wa wananchi na sekta binafsi katika kuchangia maendeleo ya sekta hiyo huku ikizingatiwa mipango mikuu ya maendeleo kitaifa na kimataifa.

Lakini kazi maalum ambayo Serikali ilijipangia katika kuimarisha sekta ya afya kuanzia mwaka 2010, ilikuwa ni kuimarisha huduma za hospitali kuu ya Mnazi Mmoja, ili ifikie hadhi ya kiwango cha Hospitali ya rufaa, Hospitali ya Abdalla Mzee na Wete Pemba zifikie hadhi na kiwango cha hospitali za Mkoa na Cottage Hospital ya Micheweni na Vitongoji Pemba na Makunduchi na Kivunge, Unguja zifikie hadhi na kiwango cha hospitali ya Wilaya.

Dhamira ya Serikali kuendelea kuimarisha sekta ya afya imeendelea kuonekana kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2015 – 2020. Pamoja na mambo mengine, Serikali imepanga kuendelea kuifanya hospitali ya Mnazimmoja kuwa ya rufaa kwa kuongeza huduma za matibabu ya aina mbali mbali ikiwemo huduma za matibabu ya saratani na huduma za uchunguzi na ununuzi wa vifaa kama vile “Magnetic Resonance Imaging” (MRI), DNA pamoja na kuongeza Idadi ya madaktari bingwa wa fani mbali mbali.

Vile vile Serikali kwenye Ilani ya CCM mwaka 2015 – 2020 imedhamiria kuendeleza jitihada zake za kuimarisha huduma za Afya ya Mama na Mtoto kwa kujenga majengo mapya ya wodi ya wazazi na wodi ya watoto katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja pamoja na kuvifanyia ukarabati vituo 19 vya afya ya msingi na kuvipatia vifaa vya kisasa Unguja na Pemba kwa lengo la kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Ni ukweli uliowazi kwamba wapo baadhi ya watu waliokuwa wakikebehi na kudhihaki mipango hiyo kama kwamba ni jambo ambalo kamwe haliwezi kutekelezeka.

Tarehe 11, Novemba 2016, wananchi wa Zanzibar, Tanzania na duniani kote walishuhudia uzinduzi wa jengo la Mama wajawazito na watoto katika hospitali ya Mnazi Mmoja, ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alikuwa mgeni rasmi.

Kwa mujibu wa taarifa ya kitaalamu iliyosomwa kwenye sherehe hiyo, ujenzi wa wodi ya watoto ulianza mwezi Disemba 2014 na uligharimu jumla ya Tsh bilioni 2.4, ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechangia Tsh 495,000,000 na fedha zilizobaki zimechangiwa na Serikali ya Norway kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Haukeland Bergen cha nchini humo.

Jengo hilo lina jumla ya ghorofa mbili na linauwezo wa kuchukua hadi vitanda 100. Linajumuisha vitengo kadhaa vikiwemo vitengo vya Wodi ya maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza, maabara ndogo kwa ajili ya watoto na kitengo cha kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo ambacho kina jumla ya mashine na vitanda 6. Vitengo vingine ni kitengo cha lishe, chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum na kitengo cha ufundi. Kimsingi jengo hili lina vifaa vyote vinavyokidhi utoaji wa huduma zilizokusudiwa.

Kwa upande wa jengo la wazazi, mradi huu umegharimu jumla ya Euro milioni 10.2 ambazo ni sawa na Tsh bilioni 25. Mradi huu



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Dk. Mariamu Abdalla Salum wakati alipotembelea Wodi ya Wazazi ya Hospitali mpya ya Abdalla Mzee baada ya kuizindua. Katikati ni balozi wa China Nchini Tanzania Lu Younqing. Uzinduzi huo umefanyika tarehe 26 Novemba, 2016

umetekelezwa kupitia ufadhili wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Uholanzi. SMZ imechangia asilimia 54 ya gharama hizo na asilimia 46 zilizobaki zimetolewa na Serikali ya Uholanzi.

Jengo la wazazi nalo lina uwezo wa kuingia vitanda 100 na linajumuisha kiasi ya vitengo 13 vikiwemo Wodi ya wazazi kabla ya kujifungua ina vitanda 42, wodi ya wazazi baada ya kujifungua vitanda 30, chumba cha kujifungulia vitanda 6, wodi ya wagonjwa wenye kifafa cha mimba vitanda 6 na vyumba viwili vya upasuaji.

Sehemu nyengine ni wodi ya watoto wachanga vitanda 8, wodi ya kangaroo (njiti) vitanda 6, kitengo cha maradhi ya dharura, chumba kidogo cha upasuaji, chumba cha X – Ray, chumba cha MRI, sehemu ya kufulia na sehemu ya mtambo wa kuzalishia oxygen.

Mradi wa ufungaji mashine ya MRI ambao unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China unatarajiwa kumalizika mwezi Januari 2017.

Lakini jambo kubwa zaidi lililoshuhudiwa na wananchi wa Zanzibar Unguja na Pemba ni tukio la kihistoria la uzinduzi wa hospitali mpya ya kisasa ya Abdalla Mzee iliyoko Mkoani, Pemba ambapo kwa mara nyengine tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alikuwa mgeni rasmi.

Hatua hiyo inafuatia upanuzi mkubwa wa Hospitali hiyo uliofanyika ili kuiongezea nafasi zaidi ya kutoa huduma. Hospitali hii mpya ina majengo manane ambayo yanajumuisha shemu ya Utawala, Jengo la huduma ya nje (OPD), Jengo la Huduma za dharura na Jengo la Huduma za Uchunguzi na upasuaji.

Majengo mengine yanajumuisha vitengo vya Huduma ya Wazazi na Watoto, Wodi za wanawake na wanaume, Jiko la kupikia, Sehemu ya kufulia na ghala ya Madawa na Sehemu ya kuchomea taka pamoja na sehemu ya kuhifadhia maiti.

Pamoja na kupanuliwa miundombinu yake, Hospitali hii vile vile imepanuliwa kwenye wigo wa utoaji wa huduma na kujumuisha huduma mbali mbali zikiwemo Huduma ya CT-Scan, mashine tatu mpya za X-Ray, Huduma za Floroscopy, Vyumba vinne vya upasuaji pamoja na huduma za Ultrasound.

Huduma nyengine ni masuala yanayohusiana na magonjwa ya moyo Electro-cardiogram (ECG), masuala yanayohusiana na maradhi ndani ya kichwa - Electro Encephalograme na huduma za uchunguzi wa maradhi – histopatholojia.

Vile vile hospitali hiyo inajumuisha utoaji wa huduma za meno ambapo kuna vitengo viwili (dental Units -02) vinavyoshughulikia masuala ya meno na chumba maalum cha wagonjwa mahututi (ICU) chenye vitanda vinne, sehemu za maradhi makali ya maambukizi pamoja na maabara ya kisasa.

Huduma zitakazotolewa katika Hospitali hii zitaweza kukidhi haja ya kutambulikana kama hospitali ya Mkoa.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dk. Juma Malik Akil, iwapo mpango ya Wizara ya Afya unaotarajiwa kuwasilishwa Serikalini hivi utakubaliwa, Wizara hiyo itaanzisha utaratibu



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Chumba cha kulelea Watoto wachanga wakati alipotembelea majengo mapya ya Wodi ya Kinamama na Watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wa pili kulia ni mwakilishi wa Ubalozi wa Uholanzi Teresia Mcha, tarehe 11 Novemba, 2016.

maalum wa kuwapokea wagonjwa watakaokwenda kupatiwa huduma za matibabu na uchunguzi baada ya tiba zao kushindikana katika hospitali nyengine ndogo ndogo yaani utaratibu wa rufaa.

Muundo na vifaa vilivyomo katika Hospitali hii kwa hivi sasa unatoa fursa ya kuifanya Hospitali ya Abdalla Mzee iwe miongoni mwa vituo vya mafunzo kwa wanafunzi wanaosoma fani za udaktari kwa kupata fursa za mazoezi ya vitendo kwenye hospitali hiyo.

Katika kuijengea uwezo wa awali, Wizara ya Afya imeshachukua hatua maalum ya kuwahamisha wafanyakazi 59 wa fani mbali mbali wakiwemo madaktari na madaktari wasaidizi 16 kutoka Unguja, na zoezi hilo litaendelea hatua baada ya hatua kadri huduma zinazotolewa zitakavyokua zikiongezeka. Vile vile, juhudi za kupata nyongeza ya madaktari kutoka China kupitia program maalum ya uletaji wa madaktari na wataalam wengine nchini zimeanza kuchukuliwa.

Kwa kuanzia Hospitali hiyo itakua na jumla ya wafanyakazi 163 wa kada mbali mbali ikiwemo madaktari 26, madaktari wasaidizi 4, wauguzi 49, wataalam wa maabara 9, wafamasia 4, Wataalamu wa nusu kaputi 4 na "biotechnologist" mmoja pamoja na kada nyenginezo. Lengo kufikia jumla ya wafanyakazi 227.

Wafanyakazi wote waliotoka Unguja tayari wameshapatiwa makaazi ya muda katika nyumba zilizokodiwa katika maeneo mbali mbali ya Mkoa Kusini (P), wakati mchakato wa ununuzi wa mabasi ya kuwasafirishia nao ukiwa umeanza. Sambamba na hatua hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tayari imeanza mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kudumu za wafanyakazi ndani ya eneo la Hospitali.

Kumalizika kwa majengo ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Hospitali ya Abdalla Mzee na kuwekwa vifaa vyote vitakavyowezesha kufanyika kazi kwa ufanisi, siyo tu kunathibitisha ukweli wa utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Serikali kwa wananchi, lakini pia kunathibitisha dhima iliyonayo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa wananchi wake.

Kwa mafanikio hayo tiba za kubahatisha ambazo zilisababishwa na kutokuwa na uhakika wa maradhi yanayowasumbua wagonjwa yamebaki kuwa historia kutokana na vifaa vya kisasa kutambua kiini cha maradhi ya mgonjwa na kuelekeza aina ya matibabu yanayofaa kwa maradhi husika.

Bila ya shaka haya ni mapinduzi makubwa katika huduma hii muhimu kwa maisha ya mwanadamu.

# Washirika wa maendeleo wanavyosaidia Zanzibar




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipokea zawadi kutoka kwa Mwakilishi wa Ubalozi wa Uholanzi Bibi Teresia Mcha katika sherehe ya ufunguzi wa majengo mapya ya Wodi za Kinamama na Watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, tarehe 11 Novemba, 2016

Tarehe 11 Novemba, 2016 Zanzibar ilishuhudia kuimarika kwa huduma za Mama wajawazito na watoto katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja baada ya kuzinduliwa rasmi Wodi ya Watoto na Wodi ya Wanawake. Wodi hizi ni za kisasa na zenye huduma bora zaidi ikilinganishwa na hospitali nyingi nchini.

Mradi mwingine mkubwa ni hospitali ya Abdalla Mzee huko Pemba ambayo imejengwa upya na kuwa moja kati ya hospitali bora nchini Tanzania. Hospitali hii ilifunguliwa tarehe 26 Novemba, 2016.

Miradi hii ambayo ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein imejengwa kwa ushirikiano mkubwa kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wa maendeleo na watu binafsi wenye kuitakia mema Zanzibar.

Kwa hakika matukio haya mawili ya uzinduzi wa Miundombinu hiyo ya afya imezidi kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Serikali ya kuimarisha huduma za afya kwa kuwapatia wananchi huduma bora na kwa wepesi.

Katika miradi yote hiyo mbali ya kujengwa majengo ya kisasa yaliyowekewa vifaa na nyenzo nyingine za kisasa ambazo sio tu zinaharakisha utoaji wa huduma na kuleta ufanisi, lakini pia zinasaidia kutoa huduma za uhakika tofauti na huko nyuma mfano mashine za kufanyia uchunguzi wa maradhi.

Katika miradi yote hiyo suala la uchunguzi wa maradhi limepewa kipaumbele kwa kuwekewa vifaa vya kisasa vya uchunguzi ambavyo kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais hata katika baadhi ya nchi hazina vifaa hivyo.

Tunaamini kwamba misaada hii inatokana na washirika wa maendeleo kuvutiwa na jitihada za uongozi wa Awamu ya Saba katika kuimarisha sekta ya afya na kuridhishwa kuwa misaada wanayoitoa inatumika vizuri na kugusa wananchi ambao ndio walengwa wakuu.

Kwa hivyo tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za kuimarisha mashirikiano na nchi marafiki na washirika wa maendeleo ambao wamedhihirisha kuridhika kwao na uongozi wake.

Katika mazungumzo yake na viongozi wa nchi mbali mbali, mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya maendeleo ya kimataifa, Mheshimiwa Rais amekuwa akieleza wazi wazi dhamira ya kweli ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Saba ya kuimarisha huduma za afya nchini na kubainisha uwezo wake na changamoto zinazoikabili Serikali yake.

Serikali yake imekuwa ikionesha kwa vitendo dhamira hiyo, kwa mfano kutenga fedha zaidi katika bajeti ya Serikali ili kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa wananchi pasi na malipo.



Madaktari kutoka Nchi mbali mbali wanaotoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani) wakati alipokuwa akitoa hutuba yake katika sherehe ya Ufunguzi wa Majengo mapya ya Wodi za Kinamama na Watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, tarehe 11 Novemba, 2016

Ni wajibu wetu kuwashukuru kwa dhati washirika wa maendeleo ambao wameendelea kuziunga mkono jihada za Serikali na za wananchi wa Zanzibar katika harakati zao za kujiletea maendeleo.

Ni jambo la kujivunia kuona kuwa wakati wa uzinduzi wa miradi hiyo washirika wote wa maendeleo wamemhakikishia Rais na wananchi wa Zanzibar kuwa baada ya kukamilisha miradi hiyo wako tayari kuendelea kushirikiana na Serikali katika miradi mingine kwa faida ya wananchi wa Zanzibar.

"Uholanzi imejidhatiti kutekeleza ahadi yake katika mradi huu, tumeanza pamoja na tutamaliza pamoja" alieleza Bibi Theresia Mcha Mwakilishi wa Ubalozi wa Uholanzi ambao ndio iliyotoa asilimia 46 ya gharama za mradi huo uliogharimu shilingi bilioni 25 za Tanzania.

Katika maelezo yake hayo mafupi wakati wa uzinduzi wa jengo hilo Bibi Mcha alieleza utayari wa Uholanzi wa kuendelea kusaidia Zanzibar na kueleza matumaini yake kuwa mradi huo "utakuwa mfululizo wa ushirikiano katika kutekeleza miradi mingine mingi kwa faida ya wananchi wa Zanzibar".

Wodi ya watoto imejengwa kwa msaada kutoka Serikali ya Norway ilichangia shilingi bilioni1.4 na bwana Trond Mohn mhisani kutoka nchi hiyo naye alichagia shilingi bilioni 2.2 ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa shilingi milioni 500.

Ni vyema kubainisha hapa kuwa msaada huo ni matokeo ya ushirikiano mkubwa kati ya hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland cha nchini humo.

Kama ilivyokuwa kwa Uholanzi, Norway ni mshirika mkubwa wa Zanzibar kwa miaka mingi na nchi hiyo imekuwa ikisaidia mbali ya sekta ya afya, sekta nyingine za maendeleo ikiwemo nishati, kilimo na maliasili.

Katika maelezo kwenye sherehe ya uzinduzi wa jengo hilo, Meneja wa Mradi na Mwakilishi wa Ubalozi huo bwana Victor Mlunde alieleza kuwa kupitia ushirikiano wa kimaendeleo na uwekezaji, Norway itaendelea kusaidia kujenga mustakbala mzuri kwa watoto wa Zanzibar wa sasa na wa baadae.

"Tunatarajia wodi hii itakuwa kichocheo cha kuongeza kasi ya kufikia malengo endelevu ya maendeleo ya dunia ya kupunguza idadi ya vifo kwa angalau 12 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai na vifo vya watoto chini ya umri wa miaka 5 kwa angalau 25 kwa kila watoto 1,000 ifikapo mwaka 2030" Alisema Mwakilishi huyo.

Jambo moja ambalo liliwafurahisha wengi katika uzinduzi wa wodi hiyo ni taarifa kuwa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukland itasaidia ukarabati mkubwa wa hospitali ya wagonjwa wa akili ya Kidongo Chekundu. Hii ni taarifa njema na kielelezo cha uhusiano mzuri kati ya Zanzibar na nchi hiyo. Tayari makubaliano ya awali (MOU) kuhusiana na mradi huo yameshafikiwa.

Kwa upande mwingine msaada mkubwa wa ujenzi na upanuzi mkubwa wa hospitali ya Abdalla Mzee kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ni matunda ya udugu na urafiki kati ya watu wa nchi hiyo na Zanzibar.

Kama inavyoonesha historia, kwa miaka zaidi ya 50 China imekuwa na uhusiano mzuri na wa kipekee na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo chini ya uhusiano huo Zanzibar imekuwa mshirika mkubwa.

Ikiwa ni miongoni mwa nchi za mwanzo zilizoyatambua Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964, China

imekuwa ikiisaidia Zanzibar katika sekta mbalimbali za maendeleo lakini sekta ya afya imekuwa na mashirikiano ya aina yake.

Kwa hivyo msaada wa upanuzi na ujenzi wa hospitali ya Abdalla Mzee ulitarajiwa kwa kuwa ni muendelezo wa historia hiyo ya ushirikiano katika sekta ya afya kati ya Zanzibar na China.



Baadhi ya vitanda vya kisasa vilivyomo katika Wodi ya Kinamama katika majengo mapya ya Hospitali ya Mnazi Mmoja yaliyofunguliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, tarehe 11 Novemba, 2016

Akizungumza katika sherehe za uzinduzi wa hospitali hiyo Balozi wa China nchini Mheshimiwa Dk. Lu You Quin alisema nchi yake inathamini sana ushirikiano wake na Zanzibar na kueleza kuwa miradi mingi ya maendeleo ambayo nchi hizo zimekuwa zikishirikiana kwa miaka zaidi ya 50 sasa ni kielelezo cha urafiki huo.

Alimhakikishia Mheshimiwa Rais na wananchi wa Zanzibar kuwa nchi yake itaendelea kushirikiana nao katika kutekeleza miradi waliyokubaliana sasa na itakayobuniwa baadae.

Kuhusu hospitali hiyo, balozi Lu You Quin alieleza kuwa madaktari na wataalamu kutoka China wataendelea kuwepo katika hospitali hiyo kusaidia uendeshaji wake kwa kutoa huduma kwa wagonjwa na pia mafunzo kwa madaktari na watumishi wa hospitali hiyo ili kudumu utoaji hudumu kwa vifaa vipya vilivyowekwa.

Ndio maana katika hotuba yake ya uzinduzi wa hospitali hiyo Mheshimiwa Rais alieleza kwa hisia kali namna ushirikiano kati ya Zanzibar na China ulivyokuwa ni wa kipekee katika historia ya ushirikiano wake wa kimataifa.

"Katika marafiki wetu, China ndio marafiki wetu wa kweli… asiyekujua hakuthamini, sisi tunawajuwa hivyo tunawathamini" alieleza Dk. Shein na kumshukuru kwa namna ya pekee Rais wa nchi hiyo Mhe. Xin Jinping kwa kukubali kutoa shilingi bilioni 35 kwa ajili ya ujenzi na vifaa vya hospitali hiyo.

Kama alivyoeleza katika hadhara ile msaada huo mkubwa kutoka Serikali na wananchi wa Jamhuri ya Watu wa China, umebadili historia ya huduma za afya kisiwani Pemba.

Kwa hatua hiyo, wananchi wa Pemba hivi sasa hawatakuwa na sababu ya kusafiri kwenda nje ya kisiwa hicho kupata vipimo au matibabu ambayo yatakuwa yanapatikana katika hospitali ya Abdalla Mzee.

Kwa hakika matukio haya makubwa yaliyopamba mwezi Novemba 2016 yameufanya mwezi wa Novemba 2016 kuwa wa kumbukumbu kubwa ya uongozi wa Awamu ya Saba katika historia ya maendeleo ya sekta ya afya Zanzibar.

Kwa upande mwingine, umeonesha jinsi Zanzibar inavyosonga mbele na kujiimarisha katika kuendeleza ushirikiano wake na jumuiya ya kimataifa. Kwa mnasaba huo hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongoza vyema jitihada hizo na matokeo yake yanaonekana.



Baadhi ya Wafanyakazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani) alipokuwa akitoa hutuba yake katika sherehe ya Ufunguzi wa Majengo mapya ya Wodi za Kinamama na Watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, tarehe 11 Novemba, 2016

# 3 Zanzibar sasa inaweza kutafuta, kuchimba mafuta yake



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akionesha hati ya muswada wa sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2016,baada ya kusaini hati hiyo katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Ikulu Mjini Unguja, tarehe 15 Novemba, 2016

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein tarehe 15 Novemba, 2016 alisaini Sheria Namba 6 ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar inayofungua milango kwa wawekezaji katika sekta ya mafuta na gesi asilia kuja kuwekeza Zanzibar.

Tafiti za awali zilizofanywa na mashirika ya mafuta na gesi zimeonesha kuwa Zanzibar inayo rasilimali hii na hivyo kuwa muhimu kwa kila Mzanzibari kuifahamu na kuiunga mkono.

Hata hivyo ni vyema kukiri kuwa tafiti hizo za awali hazikuwa za kina sana hivyo kusainiwa na kuanza kutumika kwa sheria hii kunatoa fursa muhimu kwa makampuni mbalimbali makubwa katika sekta ya mafuta na gesi kuja Zanzibar kufanya tafiti za kina na kwa wasaa zaidi.

Ni Sheria inayobeba dhima kubwa ya matumaini kwa wananchi wa Zanzibar. Pamoja na dhima hiyo kubwa ya matumaini, lakini utekelezaji wake na matokeo ya utekelezaji wa Sheria yanapaswa kuchukuliwa kwa tahadhari kubwa.

Kama alivyosema Mheshimiwa Rais baada ya kutia saini Sheria hiyo kuwa mafuta na gesi ni rasilimali muhimu katika kuleta maendeleo lakini pia ni sekta ambayo inaweza kuiyumbisha nchi kama haikutumika vizuri.

Uzoefu umetuonesha hatari na athari za rasilimali kama hizi kutotumika vizuri ikimaanishwa kwa faida ya wananchi wengi zilivyoathiri utulivu na utengamano katika baadhi ya nchi duniani.

Dhana ya 'laana ya maliasili"(natural resource curse) imeibuliwa na wataalamu wa masuala ya migogoro inayohusisha maliasili/rasilimali baada ya kuenea kwa migogoro katika nchi nyingi ambazo zimebahatika kuwa na raslimali kama mafuta, gesi, madini na misitu yenye rasilimali ya miti adimu ya mbao.

Ni ukweli usiopingika kuwa miongoni mwa nchi zenye migogoro mikubwa hasa barani Afrika chanzo chake ni kugombea rasilimali kama hizo ambapo uzoefu umeonesha kuwa migogoro hiyo imekuwa migumu kuisuluhisha.

Migogoro hii inaweza kutokea kwa wananchi kukosa kushirikishwa na pia kutoona faida ya rasilimali hizo hasa wakati ambapo sehemu kubwa za ardhi zao zimechukuliwa kwa ajili ya shughuli hizo na hivyo kuwakosesha maeneo ya kujitafutia riziki.

Lakini kwa upande mwingine ipo hatari pia ya uchumi wa mafuta kuleta athari zisizotarajiwa kwenye sekta nyingine za uchumi kama uongozi hautakuwa makini katika kuwaelimisha wananchi umuhimu wa sekta hiyo na sekta nyengine za kiuchumi.

Mfano mkubwa hapa unatolewa kwa nchi kama Uholanzi ambayo iliathirika kiuchumi ambapo baada ya kugundua mafuta ikazipa mgongo shughuli nyingine za uchumi na kugeukia mafuta. Hali hii maarufu inajulikana kama 'ugonjwa wa kidach'(dutch disease).



Baadhi ya Mawaziri na viongozi mbali mbali wa Serikali wakiwa katika hafla ya utiaji saini mswada wa sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2016, uliotiwa saini na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika ukumbi wa Ikulu Mjini Unguja, tarehe15, Novemba, 2016

Inawezekana kuwa kuchelewa kwa Zanzibar kuingia katika sekta hii kuna faida kubwa kwa kuwa kunatoa fursa ya kujifunza uzoefu uliopatikana katika nchi nyingine na hivyo kuiendesha sekta hii kwa ufanisi na kupata tija pasi na kuingia katika migogoro na wananchi wake.

Moja ya eneo ambalo Zanzibar inapaswa kuliangalia sana ni uwiano kati ya sekta hii ya nishati (shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi) na biashara ya utalii ambayo inaweza kauthirika mara moja ikiwa kutakuwa na uchafuzi wa mazingira.

Ni bahati iliyoje kuwa kuna nchi na taasisi nyingi zenye kila aina ya uzoefu na utaalamu katika sekta ya mafuta na gesi ambazo zimeonesha kuwa ziko tayari kuisaidia Zanzibar kuisimamia sekta hiyo ipasavyo.

Wakati habari hizi njema zikizagaa katika anga ya Zanzibar wapo walioanzisha chokochoko kabla ya Mheshimiwa Rais kusaini Sheria hii kwa madai kuwa kusaini Sheria hiyo ni kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini wakaenda mbali zaidi na kuiita Sheria hiyo kuwa ni kanuni tu.

Udadisi ni jambo zuri ikiwa utakuwa na lengo la kusaidia kuleta manufaa kwa walio wengi. Katika hili huhitaji usomi uliobebea kujua kuwa haya yanayozungumza ni porojo ambazo lengo lake ni kuwatoa watu katika hoja ya msingi na kuwapeleka katika mambo yasiyo na tija.

Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia ya Zanzibar imetungwa kufuatia Bunge la Jamhuri ya Muungano kupitisha Sheria mpya ya Mafuta Namba 21 ya 2015 ambayo inabainisha usimamizi wa rasilimali za mafuta na Gesi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ni vizuri kufafanua hapa kuwa Sheria hiyo iliyopitishwa na Bunge haikuliondoa suala la mafuta na gesi katika orodha ya mambo ya Muungano kama watu wengi na hata Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilivyopendekeza.

Badala yake Sheria hiyo inaeleza kuwa rasilimali hizo zitasimamiwa na serikali ambayo kwa mujibu wa tafsiri ya Katiba ni Serikali ya Jamhuri ya Muugano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kabla ya kupitishwa Sheria hiyo, Sheria iliyokuwepo ilikuwa inalipa mamlaka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) pekee kushughulikia masuala hayo.

Kwa mantiki hiyo suala la kuvunja Katiba halipo kwa kuwa bado suala la mafuta na gesi limebaki ndani ya orodha ya mambo ya muungano ndio maana tunasema hayo maneno ya kuvunja Katiba ni chokochoko tu za watu wasioitakia mema Zanzibar na kwamba "wanajitafutia umaarufu tu" kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein mara baada ya kutia saini sheria hiyo.

Kifungu cha 2 kifungu kidogo cha 2 (a) na (b) cha Sheria Namba 21 ya 2015 kinaeleza utaratibu mzima wa kusimamia rasilimali hizo zikiwa Tanzania Bara na zikiwa upande wa Zanzibar. Kifungu hicho cha 2 kifungu kidogo cha 2(a) kinaeleza kuwa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia zikiwa zinafanyika Tanzania Bara zitasimamiwa na taasisi zilizoanzishwa kwa sheria hiyo au kutajwa katika Sheria hiyo Namba 21 ya mwaka 2015.

Ama kwa shughuli kama hizo ambazo zinafanyika Zanzibar, kifungu cha 2 kifungu kidogo cha 2 (b) kinasema kuwa zitasimamiwa kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar na hapa ndipo ilipolazimu Baraza la Wawakilishi kutunga Sheria Namba 6 kuipa Zanzibar mamlaka ya kisheria kusimamia vyema rasilimali hii.

Sheria hii imeweka wazi jinsi mapato yatokanayo na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Kifungu cha 4(a)na (b) cha Sheria vinatamka kuwa kwa upande wa Tanzania Bara mapato yatatumiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa faida ya Tanzania Bara wakati kwa upande wa Tanzania Zanzibar mapato hayo yatatumiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa manufaa ya Zanzibar.

Katika hali hii, Sheria hii imeyaangalia na kuzingatia maslahi ya pande zote Tanzania Bara na Zanzibar. Kila upande umepata kilicho chake na kinachostahiki kwa mujibu wa sheria. Tunasema hivyo kwa kuwa kila mmoja atafanya shughuli zake ndani ya mipaka yake na kunufaika kwa kadri atakavyoona inafaa na wananchi wake. Kwa hivyo, chokochoko za nini?

Wito kwa wazanzibari wote ni kuwataka waimarishe udugu wao, upendo na mshikamano wao na kuiunga mkono serikali kwa kushirikiana nayo kujenga mazingira mazuri ya kuitekeleza Sheria hii kwa kuzingatia maslahi mapana ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

4

# Wanawake Zanzibar wamethibitisha wanaweza



Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akiwa katika picha ya pamoja na Wake wa Viongozi, Wawakilishi pamoja na Viongozi wa Chama na Serikali mara baada ya kikao chao kilichofanyika katika ukumbi wa Ikulu ya Chake Chake Pemba, tarehe 08 Novemba, 2016

Takriban miaka 21 sasa tokea mwezi Septemba mwaka 1995 ulipofanyika mkutano mkuu wa nne wa Umoja wa Mataifa mjini Beijing, ambao ulipitisha azimio la kutambua usawa wa kijinsia, azimio ambalo lilitoa fursa zaidi kwa akinamama kuwa na ushiriki sawa na wanaume katika kufikia maamuzi yote muhimu ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Tokea kumalizika mkutano huo, mataifa mengi duniani yamekuwa yakichukua hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya katiba zao kuhakikisha kuwa wanatekeleza azimio hilo.

Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwenye katiba haki na usawa kwa kila mtu bila ya kujali jinsia, dini kabila, uzawa au aina yoyote ya ubaguzi. Kifungu cha 12 (1) cha katiba ya Zanzibar kimeeleza wazi kwamba "watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria".

Kwa kutambua na kuthamini nafasi na mchango wa wanawake katika maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Ilani yake ya Uchaguzi 2015 – 2020, imeeleza kuwa itahakikisha kuwa inaendelea kupiga vita mila, desturi na sheria zinazowabagua wanawake pamoja na kusimamia sheria na mikataba ya Kimataifa inayohusu haki na ustawi wa wanawake.

Aidha, CCM kimesema kitaendelea kuhamasisha na kushajiisha juu ya kuwepo na fursa sawa bila kujali jinsia katika elimu, nafasi za uongozi, na utawala sambamba na kuhamasisha taasisi za fedha ili kuwawezesha wanawake kiuchumi.

Ingawa kulionekana kuweko na kusitasita katika utekelezaji wa azimio hilo la Umoja wa Mataifa kwenye baadhi ya nchi duniani, Zanzibar na Tanzania kwa jumla imeonekana kuweko mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko ya kiuongozi kwa kutoa fursa maalum kwa wanawake kwenye mabaraza ya kutunga sheria; bunge kwa upande wa Tanzania Bara na Baraza la Wawakilishi kwa Zanzibar. Maamuzi ya mabaraza hayo ni muhimu kuliko maeneo mengine kutokana na kugusa maisha ya kila mtu. Uamuzi huo ulichukuliwa kutokana na ukweli kwamba miaka mingi iliyopita wanawake walibaki nyuma kimaendeleo

Lakini kazi kubwa iliyofanywa

na Serikali katika utekelezaji wa azimio hilo ni kuwashajiisha wanawake kushiriki wenyewe katika kugombania nafasi mbali mbali za uongozi kupitia vyama vya siasa badala ya kusubiri nafasi za upendeleo.

Sambamba na juhudi hizo, Serikali zote mbili zimekuwa kwa muda wote zikiwapandisha daraja wanawake ambao wamekuwa wakionesha uwezo mkubwa wa kiutendaji wanapokabidhiwa dhamana kwenye ofisi au taasisi mbali mbali za Serikali.

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein ametoa pongezi za dhati kwa wanawake wote wa Unguja na Pemba kwa kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi mbali mbali za uongozi katika uchaguzi mkuu uliopita, hapa Zanzibar na Tanzania kwa jumla kuanzia nafasi ya Urais, Ubunge, Uwakilishi na Udiwani.

Akizungumza na viongozi wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT) wa Wilaya ya Mkoani katika ukumbi wa Skuli mpya ya Sekondari ya Mkanyageni Mkoa wa Kusini Pemba, Mama Mwanamwema Shein alisema ushindi uliopatikana na CCM ni muhimu sana kwa maendeleo ya wanawake na wananchi wa Zanzibar na Tanzania nzima kwa jumla kwani ushindi huo umeongeza ushiriki katika nafasi za uongozi wa juu na kuwaweka katika nafasi nzuri kwenye suala zima la kufanya maamuzi ya nchi yao.

Mama Shein alisema kuwa ni faraja kubwa kwa wanawake kuona kwamba Serikali zote mbili zilizopo madarakani hivi sasa zinahamasisha na kuunga mkono ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi kwa kuwapa nafasi mbali mbali za uongozi.

Ni wazi kwamba ushiriki wa wanawake katika siasa Zanzibar unahitaji moyo na ujasiri mkubwa kwa baadhi ya akinamama kutokana na mazingira halisi ya siasa za Zanzibar. Kwa mfano katika kipindi cha uchaguzi mkuu uliopita, kulikuwa na tishio la baadhi ya ndoa kuvunjika kutokana na tofauti za kiitikadi baina ya wanandoa. Pamoja na changamoto hiyo, wapo wanawake waliokuwa majasiri na kukubali kukabiliana na chochote kitakachotokea mradi tu watekeleze haki yao ya kikatiba ya kuchagua na pia kuchaguliwa. Ujasiri huo umethibitisha kuwa wanawake wa Zanzibar wanaweza bila ya kuwezeshwa.

Kutokana na changamoto hizo, Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein aliwapongeza wanaweke wote wa Unguja na Pemba waliojitokeza katika kuwania nafasi mbali mbali za uongozi katika uchaguzi Mkuu uliopita, kuanzia nafasi ya urais, ubunge, uwakilishi, na udiwani.

Pongezi maalum amezitoa kwa wanawake wote waliojiotokeza kuwania nafasi hizo na wakaweza kuibuka kuwa washindi. Ushindi wao ambao ni muhimu kwa maaendeleo ya wanawake wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla, umeongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi wa juu na umewaweka nafasi nzuri katika suala zima la kufanya maamuzi muhimu ya nchi yao.

"Ni faraja kubwa kwetu kuona kwamba Serikali zetu zote mbili zilizopo madarakani hivi sasa zinahamasisha na kuunga mkono ushiriki wa wanaweke katika nafasi za uongozi kwa kuwapa nafasi mbali mbali za uongozi". Alisema Mama Mwanamwema.

Vile vile, amewapongeza wanawake wote wa Unguja na Pemba waliojitokeza kwa wingi kwenda kuitumia haki yao ya msingi ya Kikatiba ya kupiga kura, licha ya baadhi yao kukumbana na vitisho vya aina mbali mbali katika familia zao. Jukumu lililo mbele ya wanawake hivi sasa ni kuzidi kujiweka tayari kushiriki kikamilifu katika chaguzi zote kupitia kwenye vyama vyao vya siasa.

"kazi iliyo mbele yetu hivi sasa, tunapaswa kujipanga tukiongozwa na UWT na kuhahikisha kwamba tunajitokeza kwa wingi na kwa ari kubwa zaidi katika kugombania nafasi mbali mbali za uongozi katika ngazi zote katika Uchaguzi Mkuu wa Chama Chetu unaotarajiwa kufanyika mwaka 2017". Alisema Mama Mwanamwema.

Takwimu zinaonesha kuwa Idadi ya wanawake nchini Tanzania ni kubwa zaidi ikilinganishwa na wanaume, hivyo hakutakuwa na ubaya wowote kuwa na idadi kubwa zaidi ya wanawake kuliko wanaume kwenye nafasi za uongozi serikalini na hata kwenye jamii, iwapo tu watakaochaguliwa au kuteuliwa kushika madaraka watakuwa na uwezo wa kutosha wa kufanyakazi wanazopangiwa na kutekeleza majukumu wanayopewa.

Mama Shein alitoa shukurani kwa uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kutoa nafasi nyingi za uongozi kwa vijana na wanawake na kutoa wito kwa akina mama wenzake kuendelea kuwa watendaji wazuri, wenye bidii na uadilifu.



Baadhi ya wake wa wawakilishi wakiwa katika kikao maalum pamoja na Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein. Kikao hicho kilifanyika katika ukumbi wa Ikulu ya Chake Chake Pemba, tarehe 08 Novemba, 2016

# Matukio mbali mbali katika Picha



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akiangalia bidhaa mbali mbali kwenye Kongamano la siku moja kuhusu Biashara baina ya Tanzania na Comoro katika ukumbi wa Sea Cliff Mangapwani Wilaya ya Magharibi "A" Unguja, tarehe 19 Novemba 2016



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifuatana na Waziri wa Afya Mhe. Mahmoud Thabit Kombo pamoja na viongozi wengine mara alipowasili katika uzinduzi wa majengo mapya ya Wodi ya Kinamama na Watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, tarehe 11 Novemba, 2016



Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akimkabidhi kadi mwanachama mpya wa UWT Wilaya ya Mkoani Bi. Biubwa Ridhiwani, hafla hiyo imefanyika katika ukumbi wa skuli ya Wilaya Mkoani Pemba, tarehe 05 Novemba, 2016



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Ujumbe kutoka Nchini Norway ukiongozwa na Bw. Eivind Hansen, Ofisa Mtendaji Mkuu kutoka Chuo Kikuu cha Haukeland walipofika Ikulu Mjini Unguja tarehe 10 Novemba, 2016



Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akipokea zawadi kutoka kwa Mwakilishi wa Ubalozi wa Uholanzi Bibi Teresia Mcha katika sherehe ya ufunguzi wa majengo mapya ya Wodi ya Kinamama na Watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, tarehe 11 Nonemba, 2016



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza kitu na Katibu Mkuu wa Wozara ya Afya Dk. Juma Malik Akili wakati walipokuwa wakitembelea sehemu mbali mbali ya Hospitali Mpya ya Abdalla Mzee, Mkoani Pemba iliyozinduliwa rasmi tarehe 26 Novemba, 2016

# Mahakama zatakiwa kuzingatia haki, usawa

5




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifunua kitambaa kuashiria ufunguzi rasmi wa Jengo la Mahakama Kuu liliopo Chake Chake Pemba kufuatia kukamilika kwa ukarabati mkubwa wa mahakama hiyo. Sherehe za ufunguzi wa Mahakama hiyo zilifanyika tarehe 5 Novemba, 2016

Jengo la Mahakama Kuu Chake Chake Pemba ni moja kati ya majengo makongwe katika mji huo ulioko katikati ya Kisiwa cha Pemba. Jengo hilo lililojengwa mwaka 1920 limefanyiwa ukarabati mkubwa ili kuimarisha mazingira ya kazi na kuleta ufanisi katika Mahakama hiyo.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa jengo hili ni moja kati ya majengo machache yaliyobaki ambayo ni sehemu ya alama za mji wa Chake Chake. Pembezoni mwa jengo hilo lipo jengo jingine mashuhuri linaloitwa Jumba la Jan (Jan building). Ukarabati mkubwa wa jengo hili ambalo lilianza kutumika mwaka 1922 umeupa mji wa Chake Chake haiba mpya.

Kama ilivyoelezwa hili ni jengo la Mahakama Kuu; mmoja wa mihimili mitatu ya dola baada ya Serikali na chombo cha kutunga sheria yaani Baraza la Wawakilishi. Hivyo ni mhimili ambao jamii imeweka matumaini yao makubwa iwe mtu mmoja mmoja, kikundi, taasisi na hata serikali yenyewe kwa kuwa ndio chombo cha kutafuta haki kwa waliokosa au walionyimwa.

Kwa hivyo uzinduzi wa jengo hili uliofanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein tarehe 05 Novemba, 2016 lilikuwa ni tukio kubwa na la historia kwa Mahakama hiyo Zanzibar.

Ni historia kwa sababu kwanza kama alivyoeleza Jaji Mkuu Mheshimiwa Omar Othman Makungu kuwa kukamilika ukarabati huo kwake yeye kunampa fursa ya kuteua Jaji Mkaazi ingawa alisema "akiona inafaa".

Hapana shaka yoyote Mheshimiwa Jaji Mkuu atazingatia haja ya kuwa na jaji Mkaazi kisiwani Pemba ili kuondoa usumbufu wa mashauri kuchelewa kusikilizwa kwa kusibiri majaji watoke Unguja ambao wanakuja kwa msimu.

Sisi tunaamini hivyo kwanza kutokana na hatua hiyo kwenda sambamba na mkakati wa Mahakama wa kupambana na mrundikano wa kesi katika mahakama zetu ikiwemo Mahakama Kuu ambao ni moja ya masuala wanayoyalalamikia wananchi kwa miaka mingi.

Kwa upande mwingine kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya uzinduzi kuwa mfumo wa sasa wa kupeleka



Mrajisi wa Mahkama Kuu Jaji George Kazi akitoa maelezo kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein mara baada ya uzinduzi wa jengo la Mahakama Kuu ya Mjini Chake Chake Pemba tarehe 5 Novemba, 2016. Kushoto ni Jaji Mkuu wa Zanzibar Mheshimiwa Omar Othman Makungu

majaji Pemba kwa kipindi maalum una changamoto zake kiutendaji ikiwemo gharama kubwa pamoja na kuchelewesha haki.

Aidha, Mheshimiwa Jaji Mkuu kumteua Jaji Mkaazi kisiwani Pemba atakuwa ametekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais yanayozitaka wizara, Idara na Taasisi za serikali kuwa na wawakilishi wao katika ofisi za Pemba.

Maelekezo hayo yanaitaka kila idara lazima iwe na mtumishi au watumishi wake watakaokuwa na jukumu la kutekeleza majukumu ya idara kiswani Pemba kwa hivyo uwepo wa Jaji Mkaazi katika Mahakama Kuu Chake Chake ni jambo lisiloepukika.

Ni jambo zuri kuona kuwa Mahakama Kuu imesimamia vizuri ukarabati huu mkubwa wa jengo hilo ambapo kwa mujibu wa taarifa ya Mrajis wa Mahakama hiyo Mheshimiwa Jaji Joseph Kazi katika kumbukumbu zao hakuna matengenezo kama hayo yaliyowahi kufanyika tokea jengo hilo lilipoanza kutumiwa mwaka 1922.

Jambo moja muhimu ambalo limefanyika na ambalo tunapaswa kuupongeza uongozi wa Mahakama ni kuweka chumba cha Mahakama ya watoto katika jengo la Mahkama hiyo ili kesi za watoto ziweze kufanyika katika mazingira mazuri na rafiki kwa watoto.

Aidha, ujenzi wa jengo dogo nao unapaswa kupongezwa kwa kuwa jengo hilo limetoa nafasi kwa idara nyingine zinazoshirikiana na Mahakama kupata nafasi ya kutekelezea majukumu yao ikiwemo jeshi la polisi na Ofisi ya Mkururgenzi wa Mashtaka.

Ndio maana Mheshimiwa Jaji Mkuu mwenyewe alikiri mbele ya kadamnasi kuwa katika mazingira ya sasa hakuna sababu tena za msingi za kuchelewesha mashauri Mahakamani hapo kero ambayo ilidumu kwa muda mrefu.

Tunaamini kuwa kauli hiyo ya Jaji Mkuu inajibu baadhi ya malalamiko ya wananchi ambayo Mheshimiwa Rais katika hotuba yake aliyaeleza ikiwemo lile la "safari za nenda rudi Mahakamani" ambalo Mheshimiwa Rais alitahadharisha kuwa inaweza kuleta sintofahamu katika jamii.

Ni dhahiri kuwa wananchi wanaichukulia kwa uzito mkubwa kauli hiyo ya Mheshimiwa Jaji Mkuu kwani hilo ndilo walilotaka kulisikia kutoka kwa kiongozi huyu mkuu wa Mahakama Zanzibar.

Naamini wananchi hawana shaka yoyote na kauli hiyo ya Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa kuwa dira ya Mahakama nchini ni "Kutoa haki sawa kwa wote na kwa wakati" hivyo Mheshimiwa Jaji Mkuu alichofanya ni kuonesha na kusisitiza utayari wa Mahakama kutimiza wajibu wake katika mazingira hayo mapya yaliyoimarishwa.

Uthabiti wa kauli hiyo unasadifu hatua za Mahakama za kuimarisha utendaji kama alivyozieleza Mheshimiwa Jaji Mkuu wakati wa hotuba yake katika uzinduzi wa jengo hilo.

Hatua ya sasa ya Mahakama kujiandaa kutoka kwenye mfumo wa uendeshaji kesi na utunzaji kumbukumbu wa zamani kwenda mfumo wa digitali ni hatua muhimu katika mazingira ya sasa ambayo matumizi ya tekinolojia ya habari yamerahisisha utekelezaji wa majukumu ya kiutawala, menejimenti na kitaaluma ndani ya taasisi mbalimbali ikiwemo Mahakama.

Aidha, uamuzi wa Mahakama kutumia uzoefu wa Tanzania Bara wa uendeshaji wa kesi kwa kuweka idadi maalum ya kesi zinazotolewa maamuzi katika kipindi cha mwaka kati ya Mahakama na Majaji wa Mahakama Kuu, Mahakimu wa ngazi zote na Makadhi wa Wilaya na Mahakama za Mwanzo ni hatua nyingine muhimu ya kuimarisha ufanisi wa utendaji wa Mahakama.

Inatia moyo kuona kuwa uongozi wa Mahakama umekuwa mkweli kwa kukiri baadhi ya mapungufu yake kama vile suala la ucheleweshaji



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbali mbali wa Mahakama Kuu na kutoka taasisi nyengine za Serikali mara baada ya uzinduzi wa jengo la Mahakama Kuu Chake Chake Pemba, tarehe 5 Novemba, 2016

wa mwenendo wa mashauri na hukumu ambazo ni mojawapo ya vitu vinavyochelewesha ukataji wa rufaa.

Tunaamini kuwa Mahakama inaamini katika dhana ya kujisahihisha. Imejitathimini na kuona wapi imefanya vizuri na wapi imetetereka na ndio maana Mheshimiwa Jaji Mkuu hakuona vibaya kueleza hali halisi kwa uwazi na ukweli na kueleza namna ya kurekebisha mapungufu hayo na pia hakusita kueleza maombi yake.

Baadhi ya wachambuzi wanaona kuwa uwazi na ukweli wa Mheshimiwa Jaji Mkuu umesaidia sana kumshawishi na kumhamasisha Mheshimiwa Rais kumfanya atoe kauli nzito katika hotuba yake.

Katika hotuba yake Dk. Shein aliitaka serikali itenge fedha za kutosha kuhakikisha kuwa jengo jipya la Mahakama Kuu linalotarajiwa kujengwa huko Tunguu wilaya ya Kati, Unguja ujenzi wake unakamilishwa ifikapo mwaka 2019.

Pamoja na maelekezo hayo, Dk. Shein aliuhakikishia uongozi wa Mahakama kuwa serikali itaendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha kuwa changamoto zinazoikabili Mahakama zinapatiwa ufumbuzi hatua kwa hatua kadri uwezo wa kifedha unapoimarika.

Tunaamini kuwa uongozi wa Mahakama umefarijika sana kusikia ahadi ya Mheshimiwa Rais kuwa katika miaka minne hii wataona "mabadiliko makubwa katika mhimili huu"

Kuwa Mheshimiwa Rais anataka kuona Mahakama inakuwa na majengo ya kisasa na kuona kuna utaratibu endelevu wa kuyafanyia ukarabati majengo ya Mahakama na kuipatia vifaa kwa kuzingatia mazingira yaliyopo ni kauli inayoinua ari na moyo wa kujituma kwa watumishi wa Mahakama.

Ni kweli kuwa watumishi wa Mahakama wamekuwa wanakabiliwa na changamoto kadha wa kadha lakini pia wameshuhudia wenyewe jitihada kubwa upande wa serikali pekee na wakati mwingine kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo kuimarisha mazingira ya kazi pamoja na mafunzo ya kuimarisha weledi wa kitaaluma wa watumishi wa Mahakama.

Katika mnasaba huo, watumishi wa Mahakama katika ngazi zote hawana budi nao kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa miiko ya taaluma yao ikiwemo kutoa haki bila ya upendeleo kwa kuepuka vishawishi mbalimbali ambavyo vinaweza kuwafanya kutoa maamuzi yasiyokuwa sahihi.

Ndio maana Mheshimiwa Rais hakufanya ajizi kuwataka watumishi wa Mahakama kuanzia Majaji hadi Mahakimu kuwa lazima wawe mstari wa mbele katika kupiga vita maovu yakiwemo kupokea na kutoa rushwa.

Lakini Mheshimiwa Rais hakuishia wito wake kwa watumishi wa Mahakama pekee bali aliwataka pia wananchi wajiepushe na vitendo vya aina hiyo badala yake aliwakumbusha kuwa huduma zote katika taasisi za serikali iwe za Mahakama au penginepo ni haki yao kisheria hivyo hawapaswi kuzilipia.

Kwa mantiki hiyo tunaunga mkono rai ya Mheshimiwa Rais kwa uongozi wa Mahakama kuwa wananchi lazima waelimishwe juu ya Mahakama hizi ambazo serikali inatumia fedha nyingi kuzijenga na kuzitunza kama ilivyofanya kwa jengo hili la Chake Chake.

Kwamba wananchi wajue faida na manufaa ya serikali yao kutumia zaidi ya shilingi 621 milioni kwa kazi ya kuimarisha Mahakama hii ya Chake Chake. Wananchi wataelewa faida kwa kupata huduma nzuri toka kwa watumishi wa Mahakama hiyo. Mapokezi mazuri, lugha nzuri, msaada kwa watu ambao hawana uzoefu wa kufika au kufuatilia mashauri katika Mahakama ambao hao ndio wengi miongoni mwa wananchi wa Zanzibar.

Mambo yakiwa tofauti na hivyo yatakuwa yale aliyotahadharisha Mheshimiwa Rais kuwa majengo hayo yatabaki kuonekana kama ni "mbwembwe tu za serikali" badala ya kuhudumia wananchi. Tufanye kazi hakuna lisilowezekana.

# Mama Mwanamwema asisitiza umuhimu wa amani, utulivu



Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein akisoma hotuba yake mbele ya viongozi na waumini ya dini ya kikristo aliokutana nao katika ukumbi wa chuo cha amili vitongoji Wilaya ya Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba, tarehe 07 Novemba, 2016

Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein kwa mara nyengine tena ameungana na viongozi wengine wa Serikali na Chama Cha Mapinduzi kusisitiza umuhimu wa amani, utulivu na mshikamano miongoni mwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla ili kufikia lengo la kuwa na maendeleo endelevu.

Kauli ya mama Mwanamwema Shein ya kuwataka viongozi wa kisiasa Kisiwani Pemba hivi karibuni kuendelea kudumisha amani, utulivu na mshikamano inabeba uzito mkubwa kutokana na ukweli kwamba amani na utulivu ndio msingi wa maendeleo na kwamba bila ya amani na utulivu hakutakuwa na maendeleo.

Wito wa Mama Mwanamwema Shein umekuja wakati muafaka ambapo baadhi ya watu ndani ya jamii wamekuwa wakiyatumia makundi ya kijamii kupenyeza chuki na uhasama miongoni mwao kwa lengo la kutekeleza malengo yao binafsi kisiasa na kiuchumi.

"Kwa kuwa mimi ni mzazi, naguswa sana na hatma ya vijana wetu kuendelea kudanganywa na kudanganyika hivyo tuendelee kuwaelimisha katika majimbo yetu kuwa wakatae kutumika katika vitendo vinavyoweza kuvuruga amani, wajue kuwa uchaguzi umekwisha", alisema Mama Shein.

Watafiti wa masuala ya kisiasa wamebainisha wazi kuwa njia nzuri ya kuweza kuwatawala wanajamii ni kutumia hila zozote ambazo hatimaye zitawezesha kuwagawa na hivyo kuwa rahisi kwa watawala kujifanyia watakavyo. Hivyo kauli zozote za viongozi zinazowataka wanaoongozwa kuungana na kuwa kitu kimoja zinajenga mustakbali mwema kwa maendeleo endelevu ya jamii au taifa husika.

Kadhalika kugawanyika kwa jamii katika misingi ya kiitikadi na kiimani imekuwa ndio chanzo kikuu cha migogoro ya kijamii katika Bara la Afrika na kwengineko duniani. Kwa msingi huo, ni dhahiri kauli, vitendo na matukio yanayofanywa na baadhi ya wanasiasa nchini, vinathibitisha dhamira mbaya ya wanasiasa hao kwa maendeleo ya nchi na wananchi wake.

Kutokana na kuzingatia ukweli huo, Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein amewataka Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa



Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mama Asha Suleiman Iddi akitia saini kitabu cha wageni wakati alipofika katika ukumbi wa Kituo cha Walimu Wingwi Wilaya ya Micheweni kwa ajili ya mkutano wa kinamama wa UWT, tarehe 06 Novemba, 2016. Kulia ni Mgeni rasmi wa mkutano huo Mama Mwanamwema Shein

Pemba kuendelea kuwaelimisha wananchi na zaidi vijana na kamwe wasikubali kutumika katika vitendo vinavyoweza kuvuruga amani, huku akiwataka kuieleza jamii kuwa uchaguzi umekwisha na kwamba hakutakuwa na uchaguzi mwengine hadi mwaka 2020.

Wito huo umetolewa wakati ambapo baadhi ya wananchi wameacha kabisa kufanya kazi zitakazowasaidia kuleta maendeleo yao na kuendelea kuhubiri siasa huku wakitarajia kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwengine wa Zanzibar kabla ya mwaka 2020.

Katika maelezo yake Mama Shein, aliwataka viongozi hao kutambua kuwa nyadhifa zao moja kwa moja zinawafanya kuwa walezi na wasimamizi katika jamii inayowazunguuka. Hivyo hawanabudi kuwasisitiza wanajamii na hasa vijana juu ya umuhimu kutafuta kazi halali ikiwa ni pamoja na kujiajiri wenyewe kwani Serikali haina nafasi za kutosha za ajira kuweza kukidhi mahitaji ya vijana wote.

Tatizo ambalo limekuwa likiwaathiri vijana ni matumizi ya dawa za kulevya ambalo nalo Mama Mwanamwema Shein katika mazungumzo yake alilizungumzia kwa upana wake. Alisisitiza haja ya viongozi hao kuwaelimisha vijana juu ya madhara ya utumiaji wa dawa za kulevya na kuwataka vijana walioko skuli kuongeza bidii katika masomo yao kwani alisema nchi hii itajengwa na wananchi wenyewe hasa vijana wenye elimu, maarifa na ujuzi.

Ameeleza kuhuzunishwa kwake na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto na kuwataka viongozi hao kuchukua juhudi maalum katika kuwaelimisha vijana na wazazi juu ya mbinu za hadaa na mazingira yanayotumiwa na wabakaji na wadhalilishaji wote kwa jumla ili kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa tabia hiyo ambayo imekuwa ikiitia aibu kubwa Zanzibar.

Katika jitihada za kukabiliana na vitendo hivyo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa upande wake imeanza kuchukua hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuanzisha kampeni maalum ya kutokomeza vitendo hivyo kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na Taasisi mbali mbali na washirika wa maendeleo.

Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hilo, Serikali inaangalia uwezekano wa kuunda Kamati Maalum katika Majimbo, ambazo zitakuwa ndio kimbilio kwa wananchi pale linapotokea tatizo la udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Akizungumzia mikakati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kukabiliana na umasikini, Mama Mwanamwema Shein alisema kuwa miongoni mwa majukumu ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Saba chini ya uongozi wa Rais Dk. Ali Mohamed Shein imejipa ni kuandaa fursa mbali mbali kupitia Wizara zake, lakini viongozi nao wanawajibu wa kuwaunganisha wananchi na kuwahamasisha



Baadhi ya wajumbe wa mkutano wa kinamama wa UWT Wilaya ya Micheweni wakipiga makofu na kuimba nyimbo mbali mbali wakati wa mkutano huo uliofanyika katika ukumbi wa Kituo cha Walimu Wingwi Wilaya ya Micheweni, tarehe 06 Novemba, 2016.

kuzifuatilia na kuzitumia fursa hizo hasa kwa ajili ya akinamama na vijana.

Rai iliyotolewa na Mama Mwanamwema Shein nayo inahitaji mazingatio maalum kutokana na ukweli kwamba, akinamama wengi wamekuwa wakiziachia fursa muhimu zilizopo na kutumiwa na wanaume hata zile ambazo zimeshathibitishwa kwa vitendo kufanywa vizuri na akinamama wachache waliofanya maamuzi ya kijasiri na kuonesha mfano wa kuigwa katika siasa na uchumi.

Mafanikio ya utendaji na uaminifu wa akinamama katika nafasi nyingi za uteuzi ndani ya Serikali ya awamu ya saba, yanadhihirisha uwezo mkubwa walionao wanawake katika kufanyakazi na uwezo wao wa kutumia fursa zilizopo serikalini. Adiha, tumeshuhudia akinamama wanaofanya kazi za kupigiwa mfano kwenye fani za ukandarasi na ujasiriamali, mambo ambayo zamani yalikuwa nadra kwao.

Alitoa wito kwa akinamama kujiunga katika vikundi vya ushirika vya SACCOS na ujasiriamali kwani amesema ujasiriamali sio tu silaha muhimu katika mapambano dhidi ya umasikini, lakini njia hiyo ndio pekee itayowawezesha akinamama kujiamini katika kufanya maamuzi yao na hivyo kuondokana na utegemezi kutoka kwa akinababa.



Baadhi ya wajumbe wa mkutano wa kinamama wa UWT Wilaya ya Micheweni wakifuatilia matukio mbali mbali yaliyokuwa yakiendelea katika mkutano wao uliofanyika katika ukumbi wa Kituo cha Walimu Wingwi Wilaya ya Micheweni, tarehe 06 Novemba, 2016.

# Dakhalia zinajenga msingi imara wa elimu, maelewano



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifuatana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Riziki Pembe Juma wakitembelea sehemu mbali mbali za majengo ya Dakhalia katika Chuo cha Ufundi Kengeja, Wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba baada ya uzinduzi rasmi, tarehe 05 Novemba, 2016

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alitoa wito kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuliangalia upya suala la ujenzi wa dakhalia katika skuli za sekondari nchini. Katika Makala haya Jarida letu linaelezea kwa nini wito huu umekuja wakati muafaka.

Moja kati ya mambo yanayokumbukwa sana na wanafunzi wa zamani katika visiwa vya Unguja na Pemba na hata kwengineko ni maisha yao ya uanafunzi wakiwa dakhalia. Maisha ya dakhalia yana kumbukumbu nzuri wakati wote pamoja na visa vyake ambavyo ni sehemu ya maisha na kumbukumbu hizo.

Skuli za dakhalia zilikuwepo tangu enzi za utawala wa kikoloni ingawa zilikuwa chache kama historia ya elimu Zanzibar inavyoeleza. Baada ya Mapinduzi jitihada za Serikali za kupanua wigo wa elimu ili kutoa fursa kwa watoto kutoka familia masikini zilifanyika sambamba na kuongeza skuli zenye dakhalia.

Historia inaonesha kuwa hadi mwanzoni mwa miaka ya 1980, ni skuli chache tu Unguja na Pemba zilizokuwa zikichukua wanafunzi wa kidato cha nne au kwa maana nyingine mitihani ya kidato cha nne ilikuwa inafanyika katika skuli chache.

Wakati huo, baada ya mchujo wa kidato cha tatu, wanafunzi wengi waliochaguliwa walilazimika kwenda katika skuli hizo chache ambazo ziko mbali na nyumbani kwa mfano wanaojiunga na kidato cha nne ilikuwa ni sekondari ya Lumumba kwa Unguja na Fidel Castro kwa Pemba.

Kwa watoto waliochaguliwa kujiunga na vyuo ilikuwa chuo cha Ufundi Karume, Chuo cha Ufundi Mikunguni, Chuo cha Kiislamu na Chuo cha Ualimu Nkurumah. Vyuo hivi vyote vilikuwa Unguja.

Kwa hivyo wanafunzi kutoka kila pembe ya visiwa hivi bila kujali uwezo wao kiuchumi au jinsia walikutana katika dakhalia za Beit el Rais, kwa waliokuwa wakisoma ualimu, chuo cha Kiislamu na Lumumba na wengine walikuwa katika dakhalia ya Chuo cha Karume Mbweni. Kwa Pemba ilikuwa dakhalia ya skuli ya Fidel Castro.

Haikushangaza hata kidogo kwa Mheshimiwa Rais wakati akizindua dakhalia hiyo kutumia muda mrefu kuelezea faida za maisha ya dakhalia sio tu katika kuimarisha elimu lakini alikweda mbali zaidi na kueleza kuwa dakhalia hizo zilichangia sana kuwaunganisha vijana wa Zanzibar kuzidi kuwa kitu kimoja.

Hoja kubwa ya wakati ule ya kuwa na dakhalia ilikuwa ni kuwapatia fursa watoto walio mbali na skuli na vyuo kupata elimu kama wengine ili kuimarisha elimu na mafanikio yake yanafahamika kwa matokeo mazuri ya wanafunzi kwa kuwa walikuwa wakiishi katika dakhalia zilizokuwa na mazingira tulivu na huduma nzuri tofauti kwa walio wengi majumbani kwao.

Hata hivyo, upande mwingine wa shilingi kwa hakika faida kubwa na muhimu ilikuwa imejificha katika dakhalia hizi kwa kuwa yalikuwa ni mazingira yaliyowajenga watoto wa mashamba na mjini na wa Unguja na wa Pemba kuwa kitu kimoja na kuendeleza udugu na ukaribu wao.

Dakhalia hizi kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais zilitoa mchango mkubwa wa "kuondoa tofauti na kasumba zilizopandikizwa na wakoloni dhidi ya wananchi". Kwa walioishi katika dakhalia hizi wanakumbuka fika namna watoto walivyoishi bila ya kubaguana pasi na kuonesha tofauti za uwezo wa kifamilia au sehemu wanazotoka.

Wanafunzi wengi walijenga urafiki na kutembeleana kwa zamu wakiwa skuli na kuendeleza urafiki wao hadi katika umri mkubwa wa maisha yao. Waliweza kuendelea kujenga uhusiano mzuri katika maisha yao na kujenga mawasiliano ya karibu licha ya njia duni za mawasiliano zilizokuwepo wakati huo ikilinganishwa na wakati wa sasa ambapo njia za mawasiliano zimerahisishwa sana kutokana na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia.

Wako waliozaliwa Pemba wakiijua Unguja vizuri zaidi kuliko Pemba walikozaliwa, na vile vile wako waliozaliwa Unguja wakaijua Pemba zaidi kuliko Unguja walikozaliwa kutokana na udugu na urafiki ulioasisiwa katika maisha ya dakhalia.

Yuko mwanadakhalia mmoja alihadithia kuwa mara yake ya kwanza kuijua Pemba alikwenda katika moja ya likizo zake akiwa skuli ya sekondari kwa mwaliko wa marafiki zake wa Pemba waliokuwa wakiishi nao dakhalia.

Katika simulizi zake anasema hawezi kusahau likizo hiyo kutokana na jinsi alivyopokelewa na wenyeji wake ambapo alilazimika kuwatembelea kila mmoja kwa nyakati tofauti na kubainisha kuwa hakuweza kumaliza mialiko yote.

Ni dhahiri kuwa iko mifano mingi ya udugu na urafiki wa kweli uliozaliwa katika mazingira ya dakhalia. Kwa mfano liko kundi kubwa la wanafunzi waliosoma mchepuo katika skuli ya Fidel Castro ambalo mpaka sasa linawasiliana na kukutana wakiwa na familia zao huku wakisaidiana kwa kila kitu iwe katika furaha au huzuni.

Katika hali kama hii hapana shaka yoyote kuwa watu hawa walijenga mazingira ya kupendana na kuhurumiana na waliamini kuwa katika mazingira yale aliye karibu yako ndiye ndugu na ndiye rafiki. Na zaidi waliishi kwa kuheshimiana sana.

Ni vizuri kukumbuka kuwa umri huo ni muhimu kwa mtoto katika kumjenga kitabia iwe ya ushirikiano au ya utengano, upendo au chuki, uzalendo na kupenda nchi yake.

Hata hivyo, pamoja na faida hii ya kujenga utaifa ni bahati mbaya kuwa kadri hatua za upanuzi wa fursa za elimu zilivyopamba moto kwa kuongeza skuli zenye kutoa elimu hadi kidato cha nne na kuenea katika sehemu nyingi za Unguja na Pemba ndivyo umuhimu wa kuwa na dakhalia maskulini ulivyozidi kufifia.

Hali hiyo ilichagizwa pia na hali mbaya ya uchumi wa Zanzibar katika miaka ya mwisho wa 1980 baada ya bei ya karafuu kushuka katika soko la dunia na kusababisha uwezo wa serikali kuzihudumia dakhalia hizo kupungua sana matokeo yake dakhalia hizo kuwa na huduma duni.

Uko msemo wa lugha ya Kiswahili unaosema 'ya kale hayaji' lakini pia uko msemo wa lugha ya kingereza kuwa 'historia hujirudia'.

Kwa hivyo wito wa Mheshimiwa Rais wa kuutaka uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuangalia upya mahitaji ya dakhalia katika skuli na vyuo vyetu ni hatua muhimu. Tunafahamu kuwa tayari zipo jitihada zinazofanywa na baadhi ya vyuo vya umma za kurejesha dakhalia halikadhalika katika skuli binafsi.

Katika kuangalia umuhimu wa kuendeleza misingi mizuri ya utengamano wa watu wa Zanzibar kurejesha dakhalia ni hatua muhimu. Udugu na urafiki unaojengwa katika mazingira ya dakhalia hauwezi kujengwa katika mazingira mengine na hili halihitaji mtaalamu wa roketi kulithibitisha.

Ni jambo la kushukuru kuwa mheshimiwa Rais ameliona hilo na kulitolea tamko hivyo ni matumaini ya wananchi wa Zanzibar kuwa uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali utalifanyia kazi agizo hilo bila ajizi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Mkandarasi wa Wizara Elimu na Mafunzo ya Amali Khamis Rashid mara baada ya kuzindua majengo ya Dakhalia katika Chuo cha Ufundi Kengeja, tarehe 05 Novemba, 2016. Kushoto ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Riziki Pembe Juma

# WEMA yatakiwa kuongeza kasi elimu ya Maandalizi

8




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kuashiria uzinduzi wa madarasa mapya ya Maandalizi katika Skuli ya Gando Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba akiwa katika ziara ya kufungua miradi mbali mbali ya Maendeleo. Kulia ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Riziki Pembe Juma, uzinduzi huo ulifanyika tarehe 06 Novemba, 2016

Tarehe 6 Novemba, 2016, shehia ya Junguni katika jimbo la uchaguzi la Gando, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba iliweka historia mpya kwa kuzindua skuli ya maandalizi katika skuli ya Gando.

Skuli ya Gando ni moja kati ya skuli kongwe kisiwani Pemba. Watu wengi wamepitia katika skuli hii na inawezekana msomaji ukawa ama mmoja wa watu waliofaidika moja kwa moja na matunda ya skuli hii au miongoni mwa watu wako wa karibu wanahusiana moja kwa moja na matunda ya skuli hii. Wengi waliopitia skuli hii hivi sasa ni miongoni mwa viongozi katika taasisi mbali mbali za serikali, mashirika ya umma na vyama vya siasa.

Tukio la tarehe 6 Novemba, 2016 la uzinduzi wa skuli mpya ya maandalizi katika skuli ya Gando limeitia shehia ya Junguni katika vitabu vya historia kwa mara ya kwanza kuwa na madarasa ya kisasa ya maandalizi.

Wananchi wa shehia hiyo wameitikia kwa vitendo wito wa serikali wa kuunga mkono sekta ya elimu kwa kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya elimu na huduma nyingine katika sekta hiyo.

Kwa hivyo ni vyema kueleza hapa kuwa uamuzi wa wananchi wa shehia ya Junguni kuanzisha madarasa ya maandalizi ni sehemu ya utekelezaji wa maamuzi ya Serikali yanayotaka mfumo wa elimu Zanzibar uanzie na madarasa ya maandalizi.

Kama ilivyoeleza risala, wananchi walibuni mradi huu na waliamua kuwa na majengo yaliyotenganishwa na ya skuli ya msingi ili kuwahakikishia utulivu watoto wa elimu ya maandalizi.

Hata hivyo, kama walivyosema wahenga 'safari hatua' utekelezaji wa mradi huu kwa bahati mbaya haukufika mwisho wake hadi pale wananchi walipobahatika kupata msaada mkubwa kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Hapana shaka yoyote watoto wa shehia hiyo kwa kuandikishwa katika skuli ya maandalizi watapata msingi imara wa elimu hivyo kufanya vizuri katika elimu ya msingi, sekondari hadi elimu ya juu.

Katika mnasaba huo wananchi wa Junguni watakuwa wamewekeza vyema nguvu zao kwa watoto wao na bila ya shaka kitendo hicho kinathibitisha namna wananchi hao wanavyothamini elimu.

Kama inavyoeleza Sera ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 2006 na kama alivyosisitiza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika maelezo yake ya ufunguzi wa skuli hiyo, elimu ya maandalizi inawapa watoto msingi mzuri wa kufanya vyema wanapoingia elimu ya msingi.

Kwa mujibu wa Mpangokazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, moja ya viashiria vya matokeo ya programu hiyo ni kuleta uwiano wa idadi ya uandikishaji katika ngazi ya maandalizi na msingi.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, Zanzibar hivi sasa kuna jumla ya skuli za maandalizi 295 kati ya hizo 30 ni za serikali na 265 ni za jamii ama binafsi. Kati ya skuli za maandalizi 30 za serikali 19 ziko Unguja na 11 ziko Pemba.

Aidha, hadi Novemba 2016, kuna skuli za msingi 215 zenye

madarasa ya maandalizi Unguja na Pemba. Kati ya hizo 115 ziko Unguja na 99 ziko Pemba. Kisiwani Pemba skuli nyingine 18 za mchanganyiko Msingi na Kati pia zina madarasa ya maandalizi.

Elimu ya maandalizi hutolewa pia kupitia vituo maalum vijulikanavyo kama "Tucheze Tujifunze" maarufu TUTU. Vituo hivi kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Elimu ya Maandalizi na Msingi Bi Sofia Ali Rijali vipo katika maeneo ya vijiji vya mbali sana kutoka maeneo yenye skuli ambako watoto wadogo wa maandalizi inakuwa vigumu kuvifikia. Hadi sasa kuna vituo 299 vya TUTU kati yake 160 viko Unguja na 139 Pemba.

Kwa mwaka 2016 pekee jumla ya wanafunzi wapya 13,690 wa ngazi ya elimu ya maandalizi waliandikishwa. Kutokana na utekelezaji mzuri wa programu hii, ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi ngazi ya maandalizi ulifikia 55,731 mwaka 2015/2016 ambao ni sawa na asilimia 58.2

Shabaha ya programu hiyo kwa mujibu hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali aliyoitoa wakati wa kikao cha bajeti, ni kuongeza kiwango cha uandikishaji kutoka asilimia 58.2 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 65.0 mwaka 2016/2017.

Kwa maana hiyo wito wa Mheshimiwa Rais wa kuongeza kasi ya utekelezaji sera ya elimu katika kipengele hiki cha elimu ya maandalizi ili watoto wote waliofikia umri wa miaka minne waweze kujiunga na elimu ya maandalizi kama sera hiyo ilivyoelekeza hapana budi kuungwa mkono na kila mzanzibari na hasa kila mzazi.

Kama ilivyoelezwa kabla takwimu kisiwani Pemba zinaonesha kuwa hadi sasa kuna skuli za maandalizi za serikali 11 tu; kati ya hizo 5 ziko wilaya ya Micheweni ambazo ni Konde, Kiuyu, Ungi, Wingwi na Micheweni.

Wilaya nyingine tatu kisiwani humo kila moja ina skuli mbili za maandalizi ambazo ni Machomane na Madungu wilaya ya Chake Chake, Uweleni na Mkoani wilaya ya Mkoani na Jadida na Mitiulaya katika Wilaya ya Wete. Skuli zote hizo zikiwa na watoto 1,876.

Zipo pia skuli kama hizo binafsi (na za jamii) 42 zenye wanafunzi 3,584. Kati hizo 9 ziko Wilaya ya Micheweni, 12 Wilaya ya Wete, 13 Chake Chake na Wilaya ya Mkoani skuli 8.

Hiyo ni hatua nzuri lakini kama alivyotoa wito Mheshimiwa Rais, ni lazima kuongeza juhudi ili kusiwe na watoto wanaopaswa kuhudhuria elimu ya maandalizi lakini wanakosa kufanya hivyo kutokana na kukosekana kwa madarasa. Juhudi za makusudi ni lazima zichukuiwe ili kuhakikisha kuwa lengo la kuleta uwiano halisi wa uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya maandalizi na msingi linafikiwa.

Wakati tukiwapongeza wananchi wa shehia ya Junguni, tunapenda pia kutambua mchango mkubwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) kwa kuwaunga mkono wananchi wa Junguni.

Tunaupongeza mfuko huu kwa namna inavyoliangalia suala la kaya masikini kwa ujumla wake na azma yake ya kuziondoa kaya hizo katika hali zilizomo sasa.

Kama alivyoeleza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed kuwa ujenzi wa madarasa hayo kwa skuli hiyo ya maandalizi ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kusaidia Kaya Masikini kwa kuchangia katika miundombinu maalum ya elimu na afya.

Huu ni mtazamo chanya wa kupambana na umasikini kwa kuwa kuimarisha miundombinu maalumu kama ya maji, elimu na afya kunawapunguzia mzigo wa umasikini wananchi.

Kwa mfano katika elimu kuwawezesha watoto wanaotoka katika kaya masikini kuhudhuria masomo ni mkakati wenye maslahi mapana na ya muda mrefu katika ngazi ya kaya na taifa.

Ni jambo la kujivunia kuona TASAF-taasisi iliyoundwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongeza kasi ya maendeleo ya kijamii imekuwa, tangu awamu ya kwanza ya mradi hadi sasa katika awamu ya tatu, ikitekeleza malengo yake kwa ufanisi na kwa mafanikio makubwa kwa kugusa maisha ya kila siku ya wananchi.

Ni vyema kufafanua kuwa katika shehia ya Junguni ambayo ina wakaazi zaidi ya 2050, kaya 185 zinafaidika na mpango wa Mfuko huo wa kusaidia kaya masikini ambapo hadi sasa kaya hizo zimeshapatiwa jumla ya shilingi 105.18.

Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Joseph Abdalla Meza, mradi wa Mfuko huo kisiwani Pemba unatekelezwa katika shehia 78 ambapo jumla ya kaya zinazofaidika hadi sasa ni 14,386 ambazo tayari zimeshapatiwa jumla ya shilingi 5.760 bilioni.

Kwa hakika hizi ni hatua muhimu katika utekelezaji wa malengo ya mipango mikuu ya Maendeleo kama vile MKUZA II, Dira ya Maendeleo 2020 na Ilani ya Uchaguzi 20215-2020

Wakati tukiwashukuru TASAF kwa msaada huo ni wajibu wetu pia kuwapongeza wananchi wa shehia ya Junguni kwa kubuni mradi huu ambao sio kwamba leo umebadili sura ya elimu ya shehia hiyo bali pia kwa manufaa ya muda mrefu kwa watu wa Junguni na Zanzibar kwa jumla.



Baadhi ya wanafunzi wa Maandalizi wakiwa na Walimu wao katika sherehe ya Uzinduzi wa madarasa mapya yaliyozinduliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika Skuli ya Gando Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, tarehe 06 Novemba, 2016

# Ziara ya Dk. Shein Pemba imeongeza matumaini

9




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Wananchi wa Kijiji cha Ngomeni shehia ya Mgelema Wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba, wakati alipotembelea Ujenzi wa Barabara ya Kuyuni - Ngomeni, tarehe 07 Novemba, 2016

Ziara ya siku tano ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliyoifanya kisiwani Pemba kuanzia tarehe 5 hadi 9 Novemba 2016 imeongeza matumaini miongoni mwa wananchi wa Pemba hasa baada ya wananchi hao kupewa nafasi ya kuzungumza na kuuliza masuali ya ana kwa ana na Mheshimiwa Rais na hivyo kutumia fursa hiyo kuelezea changamoto zinazowakabili.

Ingawa utaratibu wa wananchi kupewa fursa ya kueleza shida zao na kuuliza masuali ya ana kwa ana na Mheshimiwa Rais kila anapokutana nao umezoeleka, katika ziara hiyo wananchi wa Pemba walionekana kuwa na shauku kubwa zaidi ya kujua mwelekeo wao kimaisha na kimaendeleo kutokana na kupata taarifa tofauti zenye utata hasa baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa marejeo Mwezi Machi mwaka 2016.

Katika mazungumzo yake kwenye maeneo mbali mbali, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alieleza kwa uwazi mbele ya wananchi wa Pemba kwamba uchaguzi umemalizika, hakutakuwa na uchaguzi mwengine hadi mwaka 2020 na kuwataka wananchi kuendelea kufanyakazi kwa bidii kwa kushirikiana na serikali yao iliyoko madarakani na kuzipuuza taarifa kwamba kutakuwa na serikali nyingine itakuja kuingia madarakani.

"Hakuna nchi inayoapishwa Rais mara mbili, mimi sina wasiwasi na Serikali yenu haina wasiwasi na tuko hapa kuwatumikia ili kuendeleza nchi yetu. Maneno haya yanawapotezea muda wenu tu" Dk. Shein aliwahakikishia wananchi hao na kuwataka kuendelea na maisha huku wakiwapuuza wanaoeneza uzushi huo.

Kauli ya Rais inafuatia taarifa zinazosambazwa na baadhi ya watu kwenye vikao visivyo rasmi na kupitia kwenye baadhi ya mitandao ya kijamii kwamba upo uwezekano ama wa kufanyika uchaguzi mwengine au kutangazwa Rais mwengine wa Zanzibar, jambo ambalo limekuwa likiwachanganya baadhi yao na hivyo kutokuwa na uhakika wa kuendelea na harakati zao za kujiletea maendeleo.

Lakini kubwa zaidi katika ziara hiyo ni ile fursa ya wananchi kuelezea changamoto zao ana kwa ana na Rais wao ambapo nyingi miongoni mwa changamoto hizo zilitolewa ufafanuzi na kuelezewa mikakati ya serikali katika

kukabiliana nazo. Zipo baadhi ya changamoto ambazo taasisi husika zimetakiwa kuzikabili katika kipindi maalum ili wananchi waondokane na usumbufu unaotokana na changamoto zilizotajwa.

kwa kiwango cha lami na kuiomba serikali kuwajengea kituo cha afya kwani wamesema wanalazimika kutembea masafa marefu kufuata huduma za matibabu, tatizo ambalo limebaki kuwa historia katika maeneo mengi ya Zanzibar.



Akizungumzia suala la barabara alipokuwa akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara katika maeneo tofauti kisiwani Pemba, Dk. Ali Mohamed Shein amesema pamoja na kuongezeka kwa gharama za ujenzi wa barabara, serikali itaendelea kutimiza ahadi zake za kujenga barabara ili kurahisisha usafiri kwa wananchi wa maeneo mbalimbali nchini.

Miongoni mwa barabara alizozitembelea ni pamoja na barabara ya Mgagadu-Kiwani yenye urefu wa kilomita 7.6 ambapo hadi sasa kilomita 3.1 zimeshawekwa lami. Barabara nyingine ni Mgagadu–Kwautao (5.3km), Kuyuni-Ngomeni (3.0 km) na Kipapo–Mgelema (6.0km).

Akizungumza na wananchi wa Kinazini shehia ya Kinazini, Wilaya ya Mkoani, wananchi kutoka vijiji vinavyozunguuka shehia hiyo waliishukuru serikali kwa kufanikisha ujenzi wa barabara

Aidha, wananchi hao wameiomba serikali kuongeza urefu wa barabara hiyo hadi Dikoni, ambako walisema ndiko wananchi wengi wanakoendesha shughuli zao za kila siku za kujitafutia maisha. Vile vile walielezea changamoto zinazowakabili katika kupata huduma za maji safi na salama na umeme katika baadhi ya maeneo.

Dk. Shein alikubali maombi ya wananchi hao; ombi la kutaka barabara hiyo ya Mgagadu-Kiwani yenye urefu kilomita 7.6 iongezwe hadi sehemu ya Dikoni ambako wananchi wengi wanafanya shughuli zao. Aidha, alikubali ombi la kujengwa kituo cha afya kwenye eneo hilo na kuahidi kuwa serikali itajenga kituo cha afya daraja la pili.

Amewaagiza wananchi hao kutafuta eneo la ujenzi wa kituo hicho na kuwaomba kuwa na subira hadi kumalizika ujenzi wa barabara inayoendelea hivi sasa ili kupata fursa ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu iliyoombwa kwa lengo la kuondoa usumbufu kwa wananchi hao.

Hata hivyo Dk. Shein aliziagiza wizara husika kushughulikia matatizo yaliyoelezwa na wananchi wa shehia hiyo ambayo ni pamoja na kukosa umeme na huduma ya maji safi na salama katika baadhi ya maeneo.

Akiwa katika kijiji cha Ngomeni Shehia ya Mgelema, Wilaya ya Chake Chake, wananchi wa kijiji hicho pamoja na kuipongeza serikali kujenga barabara yao kwa kiwango cha kifusi, wameiomba serikali kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwani wamesema kuna uwezekano mkubwa wa barabara hiyo kuharibiwa na mvua.

Kadhalika wananchi hao wameiomba serikali kuwajengea kituo kipya cha kuuzia karafuu kwani walisema licha ya kuwa eneo hilo ni miongoni mwa maeneo yenye kutoa karafuu nyingi Pemba, kituo kilichopo hakioani na hadhi na umuhimu wa karafuu.

Dk. Shein aliziagiza taasisi zilizoteuliwa maalum kushughulikia ujenzi wa barabara ya Kuyuni - Ngomeni kuhakikisha kuwa ujenzi wa barabara hiyo hadi kiwango cha lami uwe umekamilika ndani ya miezi 12 kuanzia kufanyika kwa ziara hiyo. Kadhalika aliitaka Wizara ya Afya kujenga kituo cha afya daraja la kwanza kijijni hapo ndani ya miezi tisa kuanzia wakati wa ziara hiyo.

Vile vile Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ameliagiza Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kuhakikisha kuwa ndani ya miezi mitatu imejenga mabanda mapya na ya kisasa ya kuuzia karafuu katika vijiji vya Ngomeni na Mgelema kama ambavyo imefanya katika vijiji vingine.

Katika mikutano hiyo Dk. Shein alirejea wito wake wa kuwataka wananchi kuuza karafuu zao ZSTC kwani kufanya hivyo wanapata faida mara mbili; kwanza kupata asilimia 80 ya bei ya zao hilo soko la dunia na pili serikali inapata uwezo wa kuimarisha huduma mbalimbali ikiwemo afya, elimu na barabara mambo ambayo wao ndio wanufaika wakuu.

